KITABU CHA II

Nchi za Ulaya zinazofanya kazi kwa pamoja

# KUOMBA HIFADHI, KUTAFUTA FAMILIA NA KUHAMA



# KARIBU!

## Hadithi hii inahusu vijana wanne — kama wewe.

Wamewasili Ulaya wakiwa salama baada ya safari ndefu.
Vijana wengine waliwasili peke yao. Wengine wao waliwasili wakiwa pamoja na familia.
Wana maswali mengi — na wanasaidiwa na watu wanaofanya kazi mahali wanapoishi.

## Hadithi hii inaweza kukusaidia pia!

**Utajifunza:**

- kile **ambacho hifadhi, kupata familia na kuhamishwa** inamaanisha
- unachotarajia
- kwa nini ni muhimu kwako kushiriki na kushirikiana na maafisa hao
- mtu anayeweza kukusaidia
- kuhusu haki zako

**Unaweza kusoma hadithi hii:**

- peke yako
- pamoja na rafiki
- pamoja na mtu anayefanya kazi hapa

## Soma kwa kasi yako. Ni SAWA kusitisha na kuendelea baadaye.

Ikiwa jambo ni gumu kuelewa, **muombe mtu yeyote akueleze**.
Mlezi wako, mfanyakazi wa kijamii au wakili wako wanaweza kukusaidia.

**MWISHONI, UTAPATA:**

- ukurasa wenye taarifa za eneo husika
- maswali ya kufurahisha
- nafasi ya kuandika maswali yako na kuongeza wawasiliani muhimu

Kwa watu walio **chini ya umri wa miaka 18 wanaowasili peke yao**, mlezi atateuliwa. Katika baadhi ya nchi, mlezi pia hujulikana kama mwakilishi.

Pia, katika baadhi ya nchi, **kuomba hifadhi** hujulikana kama **kuomba ulinzi wa kimataifa**.

Mwishowe, tambua kwamba huduma zote zinazotolewa katika vituo vya mapokezi unapoishi hazilipishwi. Ikiwa mfanyakazi atakuomba pesa, zungumza na afisa unayemwamini au mlezi wako.

# KUTANA NA WAHUSIKA
KATIKA HADITHI HII

## Mohamed

Nina umri wa miaka 17. Mimi huwa na furaha wakati mwingi. Ninapenda kuwasaidia marafiki na familia yangu wakati wowote ninapoweza. Niliwasili peke yangu wiki kadhaa zilizopita na ninamtafuta babu yangu. Nina hamu ya kuanza kufanya kazi.





## Ahmed

Nina umri wa miaka 15. Niliwasili pamoja na dada yangu mkubwa Jasmine, ambaye amekuwa akinilea tangu mama yetu alipofariki. Ninapenda kutagusana na kupata marafiki wapya. Ningependa sana kurudi shuleni haraka iwezekanavyo. Kwa sasa, ninajifunza lugha ya wenyeji wa eneo hili.

## Jasmine

Nina umri wa miaka 24. Niliwasili pamoja na kaka yangu, Ahmed, ambaye ninamlea kadri niwezavyo. Tuliwasili hivi karibuni na tunajaribu kuungana na mjomba wetu ambaye amekuwa akiishi Ulaya kwa muda. Ninapenda michezo na ninacheza vizuri sana mchezo wa mpira ya miguu.



## Adam

Nina umri wa miaka 9. Niko hapa peke yangu. Kwa sasa, nimeamua kutozungumza. Nilikumbwa na mambo mengi mabaya kabla ya kuwasili hapa. Ninahitaji muda kabla ya kuzungumza tena. Lakini mimi ni mwerevu na ninaelewa kila kitu. Mimi ni msikilizaji mzuri sana na ningependa kwenda shuleni. Ninawapenda marafiki wote wapya ambao nimepata kufikia sasa.





## Bint Ines

Mimi ni mlezi anayefanya kazi katika kituo hiki cha mapokezi. Ninajaribu kuwasaidia watoto na vijana wote wanaotafuta hifadhi kadri niwezavyo. Ninapenda kupika na inanifurahisha wakati kila mtu anapokuwa na shughuli za kufanya na kijishughulisha. Mazoezi hutufanya sote tuwe na afya nzuri kimwili na kiakili.



## Bw Fred

Mimi ni mshauri wa kisheria, ambayo ni aina ya wakili. Ninafanya kazi hapa pamoja na wenzangu wengi waliopokea mafunzo mazuri. Ninatoa taarifa na msaada kwa wakimbizi wote wanaoomba hifadhi kuhusu masuala ya kisheria na maombi yao ya hifadhi. Ninapenda kuvaa fulana zenye rangi nyingi zilizo na ujumbe.

Shukrani za dhati ziwaendee kwa wakimbizi wote wanaotafuta hifadhi waliosoma hadithi hii kabla haijachapishwa na kusaidia kuimakamilisha vyema.

Pia walisaidia kuchagua majina ya wahusika wakuu.

Shukrani pia ziendee mamlaka za nchini Malta na Uholanzi zilizowezesha majadiliano na vijana.


HABARI ZA MCHANA, BW FRED! TUKO HAPA KUULIZA MASWALI...
BILA SHAKA, INGIA!
LEO TULITAKA KUJIFUNZA NI KWA NINI PICHA NA ALAMA ZA VIDOLE VYETU ZILICHUKULIWA TULIPOWASILI?
SWALI ZURI!
MTU YEYOTE ANAPOWASILI ULAYA BILA PASIPOTI AU VISA, MAAFISA HAO WATAMUULIZA KUHUSU JINA LAKE, UMRI WAKE NA MAHALI ANAPOTOKA.
IKIWA UNA UMRI WA ZAIDI YA MIAKA 6, WATAKUPIGA PICHA PIA...
...NA KUCHUKUA ALAMA ZAKO ZA VIDOLE.
PICHA NA ALAMA ZA VIDOLE, AMBAZO PIA HUITWA DATA YA KIBIOMETRIKI, HUHIFADHIWA KWENYE MFUMO WA KOMPYUTA AMBAO UNA TAARIFA ZOTE KUHUSU WATU WANAOWASILI ULAYA.
HII HUSAIDIA MAMLAKA ZA HIFADHI KATIKA NCHI ZOTE ZA EU KUPATA TAARIFA ZAKO.
KWA HIVYO, PICHA NA ALAMA ZA VIDOLE VYANGU HUWASAIDIA KUNITAMBUA BAADAYE?


NDIYO!
TAARIFA HII HUSAIDIA MAMLAKA KUFUATILIA WATU WANAOWASILI, MAHALI NA LINI, SABABU ZAO ZA KUSAFIRI NA KAMA MTU HUYO AMEWAHI KUWA ULAYA HAPO AWALI.
JE, SI JAMBO LA KUSHANGAZA KWAMBA HAKUNA MTU MWINGINE DUNIANI KOTE ALIYE NA ALAMA ZA VIDOLE SAWA NA ZAKO?
NDIYO! ALAMA ZA VIDOLE NI ZA KIPEKEE NA HAZIBADILIKI, HATA TUNAPOZEEKA...
BW FRED, MARA TU PICHA YANGU NA ALAMA ZANGU ZA VIDOLE ZINAPOWEKWA KWENYE MFUMO WA KOMPYUTA, JE, SERIKALI YA NCHI YANGU YA ASILI INAWEZA KUPATA TAARIFA HII?
HAPANA, INAHIFADHIWA KWA FARAGHA NA HAITASHIRIKIWA NA SERIKALI YA NCHI YAKO YA ASILI. DAIMA SHIRIKIANA NA MAAFISA HAO NA UWARUHUSU KUPIGA PICHA YAKO NA KUCHUKUA ALAMA ZA VIDOLE VYAKO. UKIKATAA, INAWEZA KUSABABISHA UCHELEWESHAJI AU INAWEZA KUONEKANA NI KAMA HAUTAKI TENA KUOMBA HIFADHI.
PICHA YAKO NA ALAMA ZA VIDOLE VYAKO PIA ZINAWEZA KUSAIDIA KUPATA FAMILIA YAKO IKIWA UKO NAYO MAHALI HAPA. INAWEZA PIA KUSAIDIA KUANGALIA KAMA TAYARI UMESAJILIWA KWA AJILI YA KUPATA HIFADHI AU KWA SABABU ZA KIUSALAMA.


KILA MTU ANAYEWASILI NA KUTAKA KUOMBA HIFADHI ANAPASWA KUFANYA HIVYO KATIKA NCHI YA KWANZA ANAYOWASILI. NI MUHIMU KUBAKIA KATIKA NCHI ULIYOSAJILIWA.
WATUMAJI MAOMBI WENGINE HUJARIBU KUENDELEA KUISHI BILA MAMLAKA KUJUA.
MIMI PIA. NILIKUWA NATAKA KUMTAFUTA BABU YANGU. NILITENGANA NAYE WAKATI WA SAFARI. KWA KUWA NINA UMRI WA CHINI YA MIAKA 18, NINA MLEZI ANAYENISAIDIA. ALINISHAURI NIBAKI ENEO HILO ILI NIPOKEE MSAADA.
KUNA MASHIRIKA AMBAYO YANAWEZA KUMPATA BABU YANGU SALAMA BILA MIMI KUHAMA PEKE YANGU.
PIA, NIKIONDOKA, NIKO HATARINI YA KUPOTEZA BAADHI YA HUDUMA NA MSAADA MAHALI PENGINE KATIKA NCHI NYINGINE.
HASWA! MLEZI WAKO DAIMA ANATAKA **KILICHO BORA KWAKO**. PAMOJA NA MAMLAKA, WANAJARIBU KUHAKIKISHA KUWA WATOTO WANAOFIKA PEKE YAO WAKO SALAMA.


IKIWA UTAENDELEA NA KUOMBA HIFADHI KATIKA NCHI NYINGINE, AMBAYO SI NCHI ULIYOFIKA KWANZA NA INAYOKUWAJIBIKA, MAMLAKA ZA NCHI HIYO ZINAWEZA KUKUREJESHA KWA NCHI YAKO YA ASILI. UNAWEZA KUKATA RUFAA DHIDI YA UAMUZI HUU.
JE, KUKATA RUFAA NI NINI?
KUKATA RUFAA KUNAMAANISHA KUTOKUBALIANA. HATA HIVYO, UNAPASWA KUELEZEA KWA NINI HUKUBALIANI. MLEZI WAKO NA WAKILI WAKO WANAWEZA KUKUSHAURI.
JE, NI SABABU GANI ZA KUTOREJESHWA KWA NCHI ULIYOKUWA HAPO AWALI?
IKIWA UNA FAMILIA KATIKA NCHI ULIYOHAMIA AU UNA HALI MBAYA YA KIAFYA NA NI LAZIMA UENDELEE NA MATIBABU ULIYOANZA...
NINAELEWA...
KWA UJUMLA, UNAPASWA KUBAKI MAHALI ULIPOWASILI KWA MARA YA KWANZA, ULIPOOMBA HIFADHI NA MAHALI ULIPOSAJILIWA. HII INAFANYA IWE RAHISI KWAKO NA KWA MAMLAKA.


...LAKINI KUSUBIRI KUNAWEZA KUWA VIGUMU ... WAKATI MWINGINE WATU WALIOTUSAIDIA KUJA HAPA HUTUOMBA TUHAME HARAKA.
EEEH... WATU WANAOTOA MAPENDEKEZO HAYA HUENDA WASIWE NA NIA NJEMA.
DAIMA ZUNGUMZA NA MTU ANAYEFANYA KAZI HAPA NA UNAYEMWAMINI KABLA YA KUFANYA MAAMUZI MAKUBWA KAMA VILE KUONDOKA KWENDA NCHI NYINGINE.
HUKU UKISUBIRI, KUJISHUGHULISHA AU KUZUNGUMZA NA FAMILIA NA MARAFIKI UNAPOKUWA UMEFADHAIKA PIA KUNAWEZA KUSAIDIA.
ENDELEA NA MASOMO YAKO...
... CHEZA MICHEZO ...
... FURAHIA!
MTOTO HAPASWI KAMWE KUFUNGASHA BEGI LAKE NA KUONDOKA. KUSAFIRI PEKE YAKO KUNAWEZA KUWA HATARI.


NINAKUBALIANA. NIKIWA NA MLEZI WANGU, NILIWASILIANA NA SHIRIKA LINALOWAUNGANISHA TENA WANAFAMILIA.
KUTAFUTA FAMILIA KUNAITWA **UFUATILIAJI WA FAMILIA.** KULETA FAMILIA PAMOJA KUNAITWA **KUUNGANISHA** FAMILIA.
TUNAPOSEMA FAMILIA, MAMLAKA KWA KAWAIDA HUZINGATIA FAMILIA YA KARIBU KAMA VILE WAZAZI, NDUGU, BABU NA NYANYA, WAJOMBA NA SHANGAZI.
JE, TUNAHITAJI TAARIFA GANI ILI KUWAFUATILIA?
... WATAULIZA MAJINA YAO, MAHALI ULIPOWAONA NA MARA YA MWISHO KUWAONA, IKIWA UNAJUA MAHALI WALIPO NA KADHALIKA...


MAJIBU YAKO YAMEANDIKWA KWENYE FOMU YA UFUATILIAJI WA FAMILIA, AMBAYO MLEZI WAKO ANAWEZA KUKUSAIDIA KUJAZA. SHIRIKA LINALOSAIDIA KATIKA UFUATILIAJI WA FAMILIA LITAKUJULISHA IKIWA WATAWAPATA.
IKIWA WEWE, FAMILIA YAKO NA MLEZI WAKO MTAKUBALIANA, MTAUNGANISHWA TENA KWA MSAADA WA MAMLAKA. IKIWA HUTAKI KUUNGANISHWA TENA NA FAMILIA YAKO, UNAWEZA USIKUBALIANE.
KWA NINI MTU ANAWEZA ASIKUBALIANE?
HUENDA MWANAFAMILIA MMOJA NI MKATILI. MAMLAKA LAZIMA ZIZINGATIE KILA WAKATI KILE KILICHO BORA NA SALAMA ZAIDI KWAKO.
NINAELEWA. EEEH... JE, NI NGUMU KUJAZA FOMU YA UFUATILIAJI WA FAMILIA?
HAPANA IKIWA UNA HATI ZINAZOHITAJIKA, KAMA VILE CHETI CHA KUZALIWA AU PICHA YAKE KUTHIBITISHA UHUSIANO WA KIFAMILIA, SHIRIKI NA MAMLAKA HARAKA IWEZEKANAVYO.
KWA HIYO, MTOTO LAZIMA ATOE HATI?
NDIYO. KATIKA MATUKIO YA NADRA, NCHI ZINGINE ZITAOMBA KIPIMO CHA KIMATIBABU, KAMA VILE SAMPULI YA DAMU AU MATE ILI KUCHUNGUZA IKIWA MNA UHUSIANO WA KINASABA.


MATE YAKO YANA TAARIFA NYINGI. UNAWEZA KUCHAGUA IKIWA UNGEPENDA KUFANYA KIPIMO HIKI AU LA. ZUNGUMZA NA MLEZI WAKO ILI KUPOKEA USHAURI.
KUWA MWANGALIFU: IKIWA MAMLAKA YANATILIA SHAKA UHUSIANO WA KIFAMILIA AU HAZINA TAARIFA ZA KUTOSHA, HUENDA WASIRUHUSU KUUNGANA TENA. BILA SHAKA, UNAWEZA KUKATA RUFAA DHIDI YA UAMUZI KAMA HUO.
BW FRED, KUUNGANA TENA KWA FAMILIA KWA KAWAIDA HUCHUKUA KIPINDI CHA MUDA GANI?
MUDA HUTOFAUTIANA. UNAHITAJI KUWA NA SUBIRA. MLEZI ATAKUPA TAARIFA MPYA.
JISHUGHULISHE, JIFUNZE LUGHA YA WENYEJI WA ENEO HILO, MUULIZE MLEZI WAKO KUHUSU SHUGHULI UNAZOWEZA KUJIUNGA NAZO.
WAKATI MWINGINE HUWA NINA WASIWASI KUWA WATU HUFIKIRI MIMI NI MJINGA NINAPOULIZA MASWALI HAYA YOTE.


NINAULIZA MASWALI MENGI. JE, UNADHANI MIMI NI MJINGA?
BILA SHAKA HAPANA!
KUTAKA KUJUA ZAIDI KUNAONYESHA KWAMBA UKO TAYARI KUSHIRIKIANA NA MAMLAKA.
ASYLUM, FINDING FAMILY & RELOCATION
MADOKEZO
ANDIKA MASWALI YAKO NA TAARIFA AMBAZO TAYARI UMEZIPOKEA.
SASA, NATAKA KUFANYA MJARABU MDOGO PAMOJA NANYI NYOTE KUHUSU UHAMISHO KWA SABABU WAKATI MWINGINE MAMLAKA HUHAMISHA WATUMAJI MAOMBI KWENDA NCHI ZINGINE ZA EU...
VYEMA KABISA!


SWALI LA 1
NIELEZEE KUHUSU HALI AMBAPO MAMLAKA ZINAWEZA KUONDOA AU KUHAMISHA WATUMAJI MAOMBI.
WAKATI WATU WENGI WANAPOFIKA KWA WAKATI MMOJA NA HAKUNA NAFASI AU WAFANYAKAZI WA KUTOSHA KUSAIDIA.
SAHIHI!
Jasmine - 1
SWALI LA 2
WATU WANAPOHAMISHWA, JE, WANAWEZA KUCHAGUA NCHI?
HAPANA, MAMLAKA NDIYO HUCHAGUA. LAKINI LAZIMA WAZINGATIE KILICHO BORA ZAIDI KWA WATOTO. KWA SABABU HII, NI VYEMA KUWAJULISHA MAMLAKA HARAKA IWEZEKANAVYO IKIWA UNA FAMILIA BARANI ULAYA NA UNGEPENDA KUUNGANA NAO.
SAHIHI!
Jasmine - 1
Mohamed - 1
SWALI LA 3
JE, ITAKUWAJE IKIWA MTU HAKUBALIANI NA UAMUZI WA KUHAMISHWA?
UNAWEZA KUKATA RUFAA, JAMBO AMBALO LINAMAANISHA UNAONYESHA KUTOKUBALIANA KWAKO!
Jasmine - 1
Mohamed - 2
SAHIHI!

**SWALI LA 4**

**JE, UNAWEZA KUCHUKUA MUDA WAKO KUKATA RUFAA?**



# MUHIMU

**Katika nchi hii ...**

Mamlaka inayohusika na kuamua ni nchi gani inayowajibikia ombi langu la hifadhi inaitwa:

______________________________________________________________________

Ili kukutana na kuzungumza na mlezi wangu, naweza kuwasiliana na: ______________________________

______________________________________________________________________

Ninaweza kuwasiliana na mshauri wa kisheria bila malipo ili kujifunza zaidi kuhusu utaratibu wa kuomba hifadhi au kupata msaada ikiwa ninataka kukata rufaa dhidi ya uamuzi uliofanywa na mamlaka hizo.

Ili kupata ushauri kuhusu utaratibu wa kuomba hifadhi au jinsi ya kukata rufaa, naweza kuwasiliana na: ______________________________________________________

______________________________________________________________________

Ikiwa mtu yeyote anayefanya kazi hapa, kama maafisa, washauri wa kisheria, wafanyakazi wa kijamii au mlezi wangu wananitendea vibaya, ninaweza kuwasilisha malalamiko na kuwasiliana na: _________

______________________________________________________________________

Iwapo kutatokea na tukio la dharura, ninaweza kuwasiliana na huduma za ambulensi kwa

______________________________________________________________________

au polisi kwa ______________________________________________________

Mamlaka zinazohusika kuhakikisha kuwa nina mahali salama pa kulala, ambapo pia huitwa kituo cha mapokezi, zinaitwa: ______________________________________________________

Huduma zinazotolewa mahali ninapoishi hazilipishwi. Ikiwa mfanyakazi ataniomba pesa, ninaweza kuwasilisha malalamiko kwa kuwasiliana na: ________________________________________

______________________________________________________________________

# MUHIMU

**Katika nchi hii ...**

Shirika (mashirika) yanayoweza kunisaidia kutafuta wanafamilia wangu yanaitwa: ____________________
______________________________________________________________________________
______________________________________________________________________________
______________________________________________________________________________

Shirika linalohusika kunisaidia kuungana tena na familia yangu, ikiwa hii ni kwa maslahi yangu bora, ni: ______________________________________________________________________
______________________________________________________________________________
______________________________________________________________________________

Taarifa nyingine muhimu: ______________________________________________________
______________________________________________________________________________
______________________________________________________________________________
______________________________________________________________________________
______________________________________________________________________________

# MASWALI

**Ninatathmini maarifa yangu kuhusu taratibu za kuomba hifadhi!**

☑ Chagua jibu sahihi.

1. Je, ni kwa nini mamlaka zitanipiga picha na kuchukua alama za vidole vyangu na kuziweka kwenye mfumo wa kompyuta?
   - ◯ a. Kujua mimi ni nani na ni lini na mahali nilipowasili.
   - ◯ b. Kuchunguza kwa kina vidole vyangu vizuri.

2. Mamlaka hukagua ikiwa kweli nina uhusiano wa kinasaba na mtu fulani ili kuwa na uhakika kabla ya kuniunganisha tena, niko salama.
   - ◯ a. Kweli
   - ◯ b. Sio kweli

3. Haijalishi ninataka nini, mamlaka daima zitanipeleka kwa familia yangu, ikiwa nina yeyote anayeishi katika Umoja wa Ulaya (EU).
   - ◯ a. Kweli
   - ◯ b. Sio kweli (mamlaka daima zitanisikiliza mimi na mlezi ili kupata suluhisho bora kwangu katika hali yangu ya sasa.)

4. Ninaweza kuhama kwenda nchi nyingine bila matatizo yoyote wakati wowote ninapotaka.
   - ◯ a. Kweli
   - ◯ b. Sio kweli (ni bora kuzungumza na mlezi wangu kwanza ili kujua kuhusu matokeo na hatari zinazoweza kujitokeza.)

5. Nchi ya kwanza nilipoomba hifadhi na ambapo nimesajiliwa kwa kawaida ndiyo nchi inayohusika na ombi langu la hifadhi.
   - ◯ a. Kweli
   - ◯ b. Sio kweli

## Majibu ya maswali

Swali la 1: a; Swali la 2: a; Swali la 3: b; Swali la 4: b; Swali la 5: a.

# MADOKEZO

# MADOKEZO

## SWAHILI

Kijitabu hiki kinakusudiwa kutoa taarifa pekee. Hakiundi kivyake haki au wajibu wowote. Shirika la Umoja wa Ulaya wa Masuala ya Hifadhi (EUAA) limetoa sehemu kuu ya nyenzo hii, na kunakili na kufanya mabadiliko kwa kijitabu hiki kumeidhinishwa na EUAA pekee kwa Nchi Wanachama wa EU. EUAA haikubali jukumu au dhima yoyote ya usahihi, maudhui, ukamilifu, uhalali au kutegemeka kwa taarifa zilizojumuishwa katika kijitabu hiki na Nchi Wanachama wa EU au na mhusika mwingine yeyote anayewajibika. EUAA wala mtu yeyote anayefanya kazi kwa niaba ya EUAA hawajibikii matumizi yoyote yanayoweza kutokana na taarifa zilizomo katika kijitabu hiki.

© Shirika la Umoja wa Ulaya wa Masuala ya Hifadhi, 2025

